

KUMB: PPR/18 - 04/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 4 APRILI 2018

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Aprili 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Machi 2018. Kwa mwezi Aprili 2018, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 88/lita (sawa na asilimia 3.95), Shilingi 71/lita (sawa na asilimia 3.34) na Shilingi 95/lita (sawa na asilimia 4.62) sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 88.04/lita (sawa na asilimia 4.16), Shilingi 71.27/lita (sawa na asilimia 3.52) na Shilingi 95.02/lita (sawa na asilimia 4.88) sawia. Kwa kiasi kikubwa, ongezeko la bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwenye soko la ndani limetokana na mabadiliko ya bei za mafuta hayo katika soko la dunia, kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa mafuta (*BPS Premium*), kuongezeka kwa muda wa kushusha mafuta bandarini (*demurrage*) na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununua mafuta.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Machi 2018. Bei za Petroli na Mafuta ya Taa hazijabadilika kwa sababu hakuna mzungo mpya wa mafuta ya Petroli na Mafuta ya Taa ulioingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga katika mwezi wa Machi 2018. Katika toleo hili, bei za rejareja za Dizeli kwa **Mikoa ya Kaskazini** zimeongezeka kwa Shilingi 8/lita (sawa na asilimia 0.37). Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 7.81/lita (sawa na asilimia 0.39). Ongezeko la bei za mafuta ya Dizeli katika mkoa wa Tanga linatokana na kuongezeka kwa bei za mafuta hayo katika soko la dunia na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununua mafuta. Bei za mafuta ya Petroli na Mafuta ya Taa katika Mikoa ya Kaskazini kwa mwezi wa Aprili 2018 zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa katika mwezi wa Machi 2018.
- (c) Ifahamike kwamba, shehena zote za mafuta ya Petroli na Dizeli zilizopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam mwezi Machi 2018 ni zile zilizokuwa zipokelewe mwezi Februari 2018 ambazo zilinunuliwa kwa bei ya mafuta ya soko la dunia ya mwezi Januari 2018. Bei za mafuta ya Petroli na Dizeli katika soko la dunia za mwezi Januari 2018 zilipanda kwa asilimia 7.5 na asilimia 8.0, sawia ikilinganizwa na bei za mwezi Desemba 2017. Aidha shehena mbili za mafuta ya taa zilizopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam mwezi Machi 2018, ambapo shehena moja ilikuwa ipokelewe mwezi Februari 2018 ikiwa na bei ya soko la dunia ya mwezi Januari 2018, ambayo ilikuwa ni asilimia 7.7 zaidi ya bei za mwezi Desemba 2017. Shehena ya pili iliyopokelewa mwezi Machi 2018 ilinunuliwa kwa bei ya soko la dunia ya mwezi Februari 2018, ambayo ni pungufu kwa asilimia 1.4 ikilinganishwa na bei za Januari 2018.

- (d) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017.****
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,315	2,205	2,154
Arusha	2,278	2,170	1,995
Arumeru (Usa West)	2,278	2,170	1,995
Karatu	2,297	2,189	2,013
Monduli	2,284	2,176	2,000
Monduli-Makuyuni	2,288	2,180	2,005
Ngorongoro (Loliondo)	2,363	2,255	2,079
Kibaha	2,320	2,210	2,158
Bagamoyo	2,326	2,216	2,165
Kisarawe	2,323	2,213	2,161
Mkuranga	2,325	2,215	2,164
Rufiji	2,343	2,233	2,181
Dodoma	2,374	2,264	2,213

Bahi	2,381	2,271	2,220
Chemba	2,400	2,290	2,239
Kondoa	2,407	2,297	2,245
Kongwa	2,371	2,261	2,210
Mpwapwa	2,375	2,265	2,214
Iringa	2,379	2,269	2,218
Kilolo	2,384	2,274	2,222
Mufindi (Mafinga)	2,389	2,279	2,228
Njombe	2,407	2,297	2,246
Njombe (Kidegembye)	2,428	2,318	2,267
Ludewa	2,445	2,335	2,284
Makete	2,438	2,328	2,277
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,405	2,295	2,244
Bukoba	2,530	2,420	2,369
Biharamulo	2,505	2,395	2,343
Karagwe (Kayanga)	2,547	2,437	2,385
Kyerwa (Ruberwa)	2,552	2,442	2,391
Muleba	2,530	2,420	2,369
Ngara	2,496	2,386	2,334
Misenyi	2,539	2,429	2,377
Geita	2,480	2,370	2,319
Bukombe	2,469	2,359	2,308
Chato	2,501	2,391	2,340
Mbogwe	2,518	2,408	2,357
Nyang'hwale	2,495	2,385	2,334
Kigoma	2,546	2,436	2,385
Uvinza (Lugufu)	2,558	2,448	2,397
Buhigwe	2,535	2,425	2,374
Kakonko	2,503	2,393	2,342
Kasulu	2,532	2,422	2,371
Kibondo	2,511	2,401	2,349
Moshi	2,268	2,160	1,984
Hai (Bomang'ombe)	2,271	2,163	1,988
Mwanga	2,261	2,153	1,977
Rombo (Mkuu)	2,285	2,177	2,001
Same	2,254	2,146	1,971
Siha (Sanya Juu)	2,274	2,167	1,991
Lindi	2,374	2,264	2,213
Lindi-Mtama	2,392	2,282	2,231
Kilwa Masoko	2,349	2,239	2,188
Liwale	2,395	2,285	2,234
Nachingwea	2,403	2,293	2,242
Ruangwa	2,405	2,295	2,243
Babati	2,312	2,204	2,029
Hanang (Katesh)	2,323	2,215	2,039
Kiteto (Kibaya)	2,328	2,220	2,044
Mbulu	2,325	2,217	2,041
Simanjiro (Orkasumet)	2,344	2,236	2,061

Musoma	2,493	2,383	2,332
Musoma Vijijini (Busekela)	2,534	2,424	2,373
Rorya (Ingirijuu)	2,502	2,392	2,341
Rorya (Shirati)	2,537	2,427	2,376
Bunda	2,485	2,375	2,323
Butiama	2,490	2,380	2,329
Serengeti (Mugumu)	2,539	2,429	2,378
Tarime	2,505	2,395	2,343
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,509	2,399	2,348
Mbeya	2,422	2,312	2,261
Chunya	2,432	2,322	2,270
Chunya (Makongolosi)	2,446	2,336	2,284
Ileje	2,435	2,325	2,274
Kyela	2,438	2,328	2,277
Mbarali (Rujewa)	2,406	2,296	2,245
Mbozi (Vwawa)	2,431	2,321	2,270
Momba (Chitete)	2,440	2,330	2,279
Rungwe (Tukuyu)	2,431	2,321	2,270
Morogoro	2,340	2,230	2,179
Mikumi	2,356	2,246	2,194
Kilombero (Ifakara)	2,378	2,268	2,217
Kilombero (Mlimba)	2,400	2,290	2,239
Kilombero (Mngeta)	2,390	2,280	2,228
Ulanga (Mahenge)	2,389	2,279	2,227
Malinyi	2,399	2,289	2,237
Kilosa	2,359	2,249	2,197
Gairo	2,359	2,249	2,197
Mvomero (Wami Sokoine)	2,351	2,241	2,189
Turiani	2,365	2,255	2,204
Mtwara	2,388	2,278	2,226
Nanyumbu (Mangaka)	2,436	2,326	2,275
Masasi	2,413	2,303	2,252
Newala	2,420	2,310	2,258
Tandahimba	2,413	2,303	2,251
Mwanza	2,465	2,355	2,304
Kwimba	2,501	2,391	2,340
Magu	2,473	2,363	2,312
Misungwi	2,471	2,361	2,309
Sengerema	2,497	2,387	2,336
Ukerewe	2,524	2,414	2,363
Sumbawanga	2,488	2,378	2,326
Kalambo (Matai)	2,495	2,385	2,334
Nkasi (Namanyeleye)	2,501	2,391	2,340
Katavi (Mpanda)	2,523	2,413	2,361
Mlele (Inyonga)	2,501	2,391	2,340
Mpimbwe (Majimoto)	2,515	2,405	2,354
Songea	2,438	2,328	2,277
Mbinga	2,472	2,362	2,311

Namtumbo	2,468	2,358	2,306
Nyasa (Mbamba Bay)	2,474	2,364	2,313
Tunduru	2,497	2,387	2,336
Shinyanga	2,444	2,334	2,283
Kahama	2,458	2,348	2,296
Kishapu	2,472	2,362	2,311
Simiyu (Bariadi)	2,485	2,375	2,324
Busega (Nyashimo)	2,478	2,368	2,317
Itilima (Lagangabilili)	2,488	2,378	2,327
Maswa	2,477	2,367	2,315
Meatu (Mwanhuzi)	2,484	2,374	2,322
Singida	2,406	2,296	2,244
Iramba	2,418	2,308	2,257
Manyoni	2,390	2,280	2,229
Ikungi	2,401	2,291	2,240
Mkalama (Nduguti)	2,430	2,320	2,269
Tabora	2,469	2,359	2,308
Igunga	2,423	2,313	2,262
Kaliua	2,487	2,377	2,326
Ulyankulu	2,481	2,371	2,320
Nzega	2,434	2,324	2,272
Sikonge	2,481	2,371	2,320
Urambo	2,482	2,372	2,321
Tanga	2,222	2,114	1,938
Handeni	2,242	2,134	1,959
Kilindi	2,257	2,149	1,974
Korogwe	2,234	2,126	1,950
Lushoto	2,243	2,135	1,960
Mkinga (Maramba)	2,229	2,121	1,945
Muheza	2,227	2,119	1,943
Pangani	2,228	2,121	1,945

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla – DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,204.38	2,094.37	2,042.94

Bei za Jumla – TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,110.83	2,002.92	1,827.17

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA